## MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI WA KAWAIDA ROBO YA PILI OKTOBA – DESEMBA 2016 ULIOFANYIKA KWA SIKU MBILI TAREHE 27/2/2017 NA 28/2/2017 KWENYE UKUMBI WA MANISPAA TABORA

**WALIOHUDHURIA**

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. | Leopold C. Ulaya | - | Mstahiki Meya | - | Mwenyekiti |
| 2. | " | Hadija Nkumba | - | Naibu Meya | - | Mjumbe |
| 3. | " | Kananda P. Nathaniel | - | Kata ya Mbugani | - | Mjumbe |
| 4. | " | Kapela R. Shabani | - | Kata ya Isevya | - | Mjumbe |
| 5. | " | Kapemba H. Kapungu | - | Kata ya Kitete | - | Mjumbe |
| 6. | " | Juma A. Makala | - | Kata ya Ifucha | - | " |
| 7. | " | Yahaya Bakari Mhamali | - | Kata ya Mtendeni | - | " |
| 8. | | G.D. Remtullah | - | Kata ya Kanyenye | - | " |
| 9. | " | Pili Mavumbi Ally | - | Viti Maalum | - | " |
| 10. | Mhe. | Hawa Mwaifunga | - | Mbunge viti maalum | - | " |
| 11. | " | Yasini Mussa Kushoka | - | Kata ya Misha | - | " |
| 12. | " | Jumanne N. Simende | - | Kata ya Kalunde | - | " |
| 13. | " | George F. Mpepo | - | Kata ya Ng'ambo | - | " |
| 14. | " | Martin M. Daniel | - | Kata ya Mwinyi | - | " |
| 15. | " | E.L. Ndelemba | - | Kata ya Tumbi | - | " |
| 16. | " | Rehema S. Kabata | - | Kata ya Chemchem | - | " |
| 17. | " | Alphonce Shushi Kulwa | - | Kata ya Itonjanda | - | " |
| 18. | " | Zinduna S. Kisamba | - | Kata ya T/reli | - | " |
| 19. | " | Rhoda John Madaha | - | Viti Maalum | - | " |
| 20. | " | Gasham W. Mkopi | - | Kata ya Itetemia | - | " |
| 21. | " | Matama Y. Mwamba | - | Viti Maalum | - | " |
| 22. | " | Chota C. Lukuiza | - | Kata ya Kakola | - | " |
| 23. | " | Mapande M. Swalehe | - | Kata ya Kiloleni | - | " |
| 24. | " | Kitumbo Y. Hamisi | - | Kata ya Cheyo | | " |
| 25. | " | Selemani J. Maganga | - | Kata ya Ndevelwa | | " |
| 26. | " | Cornel N. Ng'wandu | - | Kata ya Malolo | | " |
| 27. | " | Waziri A. Mlenda | - | Kata ya Ipuli | - | " |
| 28. | " | Kasimu R. Kayuga | - | Kata ya Ntalikwa | - | " |
| 29 | " | Adamu I. Kalonga | - | Kata ya Kabila | - | " |
| 30 | " | Joneveva Bitakwa | - | Viti Maalum | - | " |
| 31 | " | Blandina J. Muyu | - | Viti maalum | - | " |
| 32 | " | Mlingilili S. Mrisho | - | Kata ya Mapambano | - | " |
| 33 | " | Msabaha I. Marijani | - | Kata ya K/ Chekundu | - | " |
| 34 | " | Kessy S. Abdulrahaman | - | Kata ya Gongoni | - | " |
| 35 | " | Rose C. Kilimba | - | Viti Maalum | - | " |
| 36 | | Kapeziwa M. Fundikira | - | Viti Maalum | - | " |
| 37 | " | Tausi Masoud Selemani | - | Viti maalum | | " |
| 38 | " | Hamida Omary Ally | - | Viti maalum | - | " |
| 39 | " | Toja K. Ludete | - | Viti Maalum | - | " |
| 40 | " | Salum M. Lugembe | - | Kata ya Ikomwa | - | " |
| 41 | Bw. | Bosco O. Ndunguru | - | Mkurugenzi wa Manispaa | - | Katibu |

**WASIOHUDHURIA:**

Mhe. Emmanuel Mwakasaka - Mbunge Tabora Mjini -kwa taarifa

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Mwanne Mchemba | - | Mbunge -Viti maalum -kwa Taarifa |
| Mhe. Munde A. Tambwe | - | Mbunge viti maalum - kwa Taarifa |

**WATAALAMU WALIOHUDHURIA:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bibi Novelle Mwamlenga | - | K/Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala Manispaa |
| 2. | " Abbas Mwangosi | - | Mweka Hazina Manispaa |
| 3. | " R. Mashele | - | Kaimu Afisa Biashara Manispaa |
| 4. | " W. Subuya | - | Kaimu Afisa Nyuki Manispaa |
| 5. | Bw. Ditrick Mwinuka | - | Kaimu Afisa Kilimo, mifugo na Ushirika Manispaa |
| 6. | Bw. Nasibu Rukeha | - | Katibu Tarafa Kusini |
| 7. | Bi Aziza Mgeta | - | CHAC |
| 8 | Bw. Mathias Lukala | - | Kaimu Afisa Ugavi Manispaa |
| 9 | Bw. Thomas Fue | - | Afisa elimu msingi Manispaa |
| 10 | Bw. Jonas Kilave | - | Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii Manispaa |
| 11 | Bw. Josephat Brown | - | Katibu Tarafa Kusini |
| 12 | " Josephati Lema | - | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa ndani Manispaa |
| 13 | Bi. Theodora Chuwa | - | Mwanasheria |
| 14 | "Bw. Msekwa Mbelwa | - | Afisa Habari na Mawasiliano |
| 15 | " G.A. Mwakalukwa | - | Afisa Mipangomiji Manispaa |
| 16 | Bibi Violeth Malata | - | Kaimu Afisa mifugo Manispaa |
| 17 | Bw. L. Sospeter | - | Mhandisi ujenzi Manispaa |
| 18 | " Sitta Ndamayape | - | Afisa Elimu Manispaa (S) |
| 19 | " Fadhili Chacha | - | Mratibu TASAF |
| 20 | "W. Mpangala | - | Afisa mazingira Manispaa |
| 21 | Bibi Aziza Mugeta | - | Kaimu CHAC |
| 22 | Bw. W. Kente | - | Mhasibu wa Mapato |
| 23 | " Asajile Mwandiga | - | Mhasibu wa matumizi |
| 24 | Shida Philimon | - | Kaimu Mhandisi maji |
| 25 | Oscar Lutambi | - | Kaimu Afisa Afya |

**WATENDAJI WA KATA:**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Bw. Reginald Lyimo | - | Mtendaji Kata | - | Itetemia |
| 2 | Bw. Gregory Mpena | - | Mtendaji Kata | - | Ntalikwa |
| 3 | Bw. Faida Maturino | - | Mtendaji Kata | - | Kanyenye |
| 4 | Rehema Midello | - | Mtendaji Kata | - | Mtendeni |
| 5 | Bw. Azory Kamwela | - | Mtendaji Kata | - | Cheyo |
| 6 | Bw. Robert Fashaho | - | Mtendaji Kata | - | Kakola |
| 7 | Bw. Abdallah Ng'ondi | - | Kaimu Mtendaji Kata | - | Kalunde |
| 8 | Bw.Elias Mvano | - | Mtendaji Kata | - | Mapambano |
| 9 | Bi E. Gembe | - | Mtendaji Kata | - | Uyui |
| 10 | Bi. Kalunde Omari | - | Kaimu Mtendaji Kata | - | Mbugani |
| 11 | Bibi. Veneranda Michael | - | Mtendaji Kata | - | Mpela |
| 13 | Bw. Godfrey Schalula | - | Mtendaji Kata | - | K/ Chekundu |
| 14 | Bw. Ramadhani Matandula | - | Mtendaji Kata | - | Isevya |
| 15 | Bw. Paulo Suwi | - | Kaimu Mtendaji | - | Misha |
| 16 | Bw. J.S Mbuguma | - | Mtendaji Kata | - | Kitete |
| 17 | Bw. Hamis Mlyolyo | - | Mtendaji Kata | - | Itonjanda |
| 18 | Bw. Salumu Kambi | - | Mtendaji Kata | - | Chemchem |
| 19 | Bw. Hamisi Kasonta | - | Mtendaji Kata | - | Ndevelwa |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 20 | Bw. Mohamed Mussa | - | Mtendaji Kata | - | Malolo |
| 21 | Bw. Yoel Mbwambo | - | Mtendaji Kata | - | Kiloleni |
| 22 | Bw. Nobert Mwambagi | - | K/Mtendaji Kata | - | Tumbi |
| 23 | Bw. Abbas Barunguza | - | Kaimu Mtendaji Kata | - | Ikomwa |
| 24 | Bi. Ashura Hussein | - | Kaimu Mtendaji Kata | - | Gongoni |
| 25 | Bw. Daudi Mussa | - | Kaimu Mtendaji | - | Kabila |
| 26 | Bi. Habiba S. Bandula | - | Kaimu Mtendaji | - | Ipuli |
| 27 | Bi. Neema Bugemwe | - | Kaimu Mtendaji | - | Ng'ambo |
| 28 | Bi Chiku Bunduki | - | Kaimu Mtendaji | - | Mwinyi |
| 29 | Bw. Paulo Kasembo | - | Kaimu Mtendaji Kata | - | T/Reli |

**WALIOKARIBISHWA:**

Bw. Henry Mwakyusa - TAKUKURU Mkoa
Bibi Bahati Kizee - Kny: Afisa Usalama Wilaya
Bw. Phillemon Mwaituka - Kny Mkuu wa Polisi Wilaya

**VYAMA VYA SIASA**

Rashid Ramadhani - Mwenyekiti CCM (W)
Hanati Msabaha - Katibu wa CCM (W)
Kapasha H. Kapasha - Katibu CUF Wilaya
Mirambo Kamili - Mwenyekiti CUF (W)
Msabaha E.K - Katibu CHADEMA (W)
Omari Mtwale - Mwenyekiti CHADEMA (W)

**KATIBU WA WABUNGE:**

1. Mussa Mdaki - Katibu wa Mbunge CCM
2. Kwandu Mpanduzi - Katibu wa Mbunge CHADEMA

**WAANDISHI WA HABARI :**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Hastin Luimba | Tanzania Daima |
| 2. | Saada Mohamed | Majira |
| 3. | Amina Gomba | Clouds |
| 4. | Samwel Malle | V.O.T FM |
| 5. | Vivian Pyuzya | C.G FM |
| 6. | Odale Rwimo | Mtanzania |
| 7. | Amisa Mussa | Uhuru FM Radio |
| 8 | Nicolas Kagussa | Tabora Star TV |

**FUNDI MITAMBO**

Mbogoshi Ndebile - Fundi umeme

**SEKRETARIET:**

1. J.S. Mabala - Mwandishi wa Mikutano H/ Manispaa Tabora.
2. Hussein Luziga - Mwandishi wa Mikutano H/ Manispaa Tabora.

MUHT: NA. MBM 4/2016/2017/1 - KUFUNGUA MKUTANO:

Awali ya yote Katibu alilifahamisha baraza la madiwani kwamba Mkutano huu umefanyika mwezi februari 2017 kutokana na mwezi Januari 2016 kulikuwepo na vikao vya bajeti katika Halmashauri yetu, Hivyo ililazimika baraza hili lisogezwe mbele mpaka kipindi. Vilevile Katibu alitumia nafasi hiyo kuwaomba wajumbe, wataalamu na waalikwa wote kujitambulisha.

Baada ya utangulizi huo alimkaribisha Mwenyekiti kufungua Mkutano, ambapo alifungua saa 4.17 asubuhi kwa kueleza kuwa Mkutano huu ni wa kawaida wa robo ya pili ambapo unapokea taarifa za utekelezaji za mwezi Oktoba - Desemba 2016. Alisema Mkutano huu utafanyika kwa siku mbili tarehe 27/2/2017 na 28/2/2017.

MUHT: NA. MBM 4/2016/2017/2 - KUTHIBITISHA AGENDA ZA MKUTANO

Wajumbe walipokea na kuridhia agenda zote zijadiliwe kama zinavyoonekana hapa chini:-

AGENDA ZA TAREHE 27/2/2017 SIKU YA KWANZA (1)

1. Kufungua Mkutano
2. Kuthibitisha agenda za Mkutano
3. Maswali ya papo kwa papo kwa Mstahiki Meya/Mkurugenzi toka kwa wajumbe wa Baraza la Madiwani
4. Kujadili taarifa za utekelezaji za Kata robo ya pili Oktoba _ Desemba 2016/2017
5. Taarifa ya kamati ndogo ya uchunguzi wa utekelezaji wa shughuli za miradi ya benki ya Dunia (ULGSP) katika Halmashauri ya Manispaa Tabora
6. Kuahirisha Baraza la Madiwani siku ya kwanza.

AGENDA ZA TAREHE 28/2/2017 SIKU YA PILI (2)

7.Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa Baraza la Madiwani lililofanyika tarehe 11/11/2016 na 12/11/2016
8.yatokanayo na muhtasari wa tarehe 11/11/206 na 12/11/2016
9.Taarifa ya mapato na matumizi kuishia mwezi Desemba 2016
10.Taarifa ya Mkaguzi wa ndani robo ya pili Oktoba - Desemba 2016
11.Kupokea na kujadili mihtasari ya kamati za kudumu
- (i)Kamati ya Ukimwi wa tarehe 28/10/2016
- (ii)Kamati ya Mipango Miji na Mazingira wa tarehe 31/10/2016
- (iii)Kamati ya Uchumi,Elimu na Afya wa tarehe 01/11/2016
- (iv)Kamati ya fedha na Utawala wa tarehe 02/11/2016,29/11/2016 na 13/01/2017

12. Kupokea na kupitisha maazimio ya Kamati za Kudumu
- (i)Kamati ya Ukimwi ya tarehe 13.2.2017
- (ii)Kamati ya Mipango Miji na Mazingira ya tarehe 14/2/2017
- (iii)Kamati ya Uchumi,Elimu na Afya ya tarehe 20/2/2017
- (iv)Kamati ya Fedha na Utawala ya tarehe 18/02/2017

13.Kufunga Mkutano

**MUHT: NA. MBM 4/2016/2017/3 - MASWALI YA PAPO KWA PAPO KWA MSTAHIKI MEYA/MKURUGENZI TOKA KWA WAJUMBE WA BARAZA LA MADIWANI**

Iliatolewa taarifa kwamba kuna Mhe. Diwani mmoja alikuwa amejiandikisha kwenye rejista kwa ajili ya kumuuliza Mkurugenzi maswali ya papo, kwa papo Mhe. Huyo ni Kessy Abdulrahmani toka Kata ya Gongoni.

HOJA ALIZOTOA KWENDA KWA MKURUGENZI NI KAMA IFUATAVYO:-

HOJA NA 1

Mhe. Kessy Abdulrahman - alitaka kufahamishwa kwamba ni lini sehemu ya biashara na masoko itakagua maduka yote ya biashara ili kubaini wafanyabiashara wenye leseni moja wanachanganya biashara nyingine ndani ya maduka yao mfano leseni ya duka la kawaida kuwa na vinywaji vikali,bia n.k

**Jibu** - Mkurugenzi Manispaa alipokea hoja hii kwa ajili ya kuifanyia kazi na utekelezaji utawasilishwa baraza lijalo.

HOJA NA 2

Mhe. Kessy Abdulrahman - Alitaka kufahamu ni lini wenyeviti wa Mitaa na vijiji watapewa bendera ili kuwatambulisha kwa wananchi mbalimbali, Pia alitaka kujua waheshimiwa madiwani wataandaliwa vitambulisho vyao lini?

**Jibu** -Mkurugenzi Manispaa alipokea hoja hii na kujibu kuwa suala la wenyeviti wa Mitaa na Vijiji kupatiwa bendera ataliingiza kwenye bajeti ya Halmashauri na kuhusu suala la wahe. Madiwani kuandaliwa vitambulisho alilichukua kwa ajili ya kulifanyia kazi

**MUHT: NA. MBM 4/2016/2017/4 KUJADILI TAARIFA ZA UTEKELEZAJI ZA KATA ROBO YA PILI OKTOBA - DESEMBA 2016/2017**

Wajumbe walipokea na kujadili taarifa za utekelezaji za Kata 28 ambapo walizipokea na kuzipitisha, Aidha kata moja (1) ya Uyui taarifa yake haikujadiliwa na baraza la madiwani kwa kuwa haikupitia kamati ya maendeleo ya Kata (WDC) na pia haikuwa imesainiwa na Mwenyekiti wa kamati ya maendeleo ya Kata ya Uyui ambaye alilifahamisha Baraza la Madiwani lisiijadili mpaka itakapopitia kamati ya maendeleo ya Kata.

Hivyo kutokana na hali hiyo Mhe. Diwani wa Kata ya Uyui aliliomba baraza liridhie yafanyike mabadiliko ya mtendaji wa kata aliyepo sasa na apelekwe mtendaji wa kata mwingine kutokana na aliyepo sasa Bi Imakulata Gembe kutokuonekana Ofisini mara nyingi kitu kinachosababisha Ofisi kutokutoa huduma ipasavyo kwa wananchi.

**Majibu ya Mkurugenzi Manispaa**

Alipokea suala hilo na kuahidi kulifanyia kazi

MASAHIHISHO/NYONGEZA ZILIZOFANYIKA KWENYE TAARIFA ZA UTEKELEZAJI KATA

**Mashihisho au nyongeza katika taarifa hizi yalifanyika kama ifatavyo:-**

(1)Kata ya **Mtendeni**-Sentensi iliyokuwa inasomeka ujenzi wa zahanati kata ya mtendeni umekamilika kwa asilimia 90,**ilisahihishwa** na kusomeka msingi wa zahanati kata ya mtendeni umekamilika kwa asilimia 90

(2)Kata ya Mwinyi

(i)Eneo la vijana ambalo lipo mwisho wa barabara ya lami liwekewe vibao vya kuzuia uendelezaji wa kuzika ili liendelee kubaki salama kwa ajili ya matumizi sahihi yaliyotengwa ikiwa ni pamoja na kuzuia wale wanaolima eneo lile,wasiendelee kulima

(ii)Kiwanja ambacho kimetengwa katika kata ya mwinyi kwa ajili ya ujenzi wa shule na bado hakijalipiwa fidia kwa mhusika ilipwe haraka ili kikabidhiwe katani na ujenzi wa shule mpya uanze maana tayari wananchi wanahitaji kuanza ujenzi huo,ukizingatia shule ya msingi Ally Hassani Mwinyi imegawa nywa na kuwa shule mbili katika shule moja

(3)Kata ya Gongoni- Walimpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa vita aliyoianzisha ya madawa ya kulevya

MSISITIZO

Mkurugenzi Manispaa aliwasisitiza wajumbe kwamba taarifa zinapowasilishwa wawe wanazijadili kwa kina kwa kuchangia maoni mbali mbali badala ya kuzipitisha kwani zina mambo mengi mazuri yanayohitaji kujadiliwa kwa kina na wajumbe.

MUHT: NA. MBM 4/2016/2017/5 TAARIFA YA KAMATI NDOGO YA UCHUNGUZI WA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MRADI WA BENKI YA DUNIA (ULGSP) KATIKA HALMASHAURI YA MANISPAA TABORA ILI KUBAINI NI NINI KILICHOSABABISHA MRADI HUO KUCHELEWA KUANZA KUTEKELEZWA

Kabla ya kuanza kujadili agenda hii Mstahiki Meya aliwaomba Wajumbe wajigeuze kama Kamati ya Halmashauri kwa mujibu wa Kanuni za 37 ya Kanuni za Kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Tabora za mwaka 2014 ili waweze kujadili agenda hii. Aidha aliwaomba washiriki wote wasio wajumbe watoke nje isipokuwa Wakuu wa Idara ndio wabaki ili washiriki kuijadili agenda hii kwa kina na kuitolea maamuzi.

Baada ya Waalikwa kutoka nje ya Ukumbi wa Mkutano, Mstahiki Meya alimkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Uchunguzi ili aweze kuwasilisha taarifa hiyo mbele ya Wajumbe wa Baraza la Madiwani.

Mwenyekiti alieleza kuwa Kamati ilipokea hadidu za rejea ambazo ziliainishwa kwenye barua ya uteuzi kama ifuatavyo:-

(i) Kamati ndogo ya Uchunguzi ipitie taarifa na vielelezo mbalimbali kutoka Idara husika kwa kumuomba Mkuu wa Idara/Kitengo kwa maandishi.

(ii) Kamati ndogo inayo haki ya kumhoji mtumishi yeyote kutoka Idara/Kitengo chochote kupata taarifa mbalimbali

(iii) Mtumishi anaruhusiwa kuwasilisha vielelezo mbalimbali kuhusu utekelezaji wa shughuli za miradi ya ULGSP

(iv) Kamati ndogo ya uchunguzi inapomhoji Mtumishi/Mhusika yawepo maandishi kuhusu maelezo aliyotoa na asaini kama yapo sahihi

(v) kamati iandike/ichukue orodha ya viambatanisho vya utetezi/maelezo yaliyotolewa

Aidha Mwenyekiti wa Kamati alieleza namna umbile la taarifa ya uchunguzi itakavyokuwa kwamba itakuwa na :-

- Utangulizi
- Hadidu rejea
- Maelezo ya ushahidi wa matukio halisi au masuala yaliyotokea au kuwepo
- maoni na mapendekezo ya kamati ndogo kuhusu utekelezaji wa miradi ya ULGSP
- Mazingira yote yaliyosababisha kamati ndogo itoe mapendekezo yake kuhusu kuchelewa kuanza utekelezaji/kutotekelezwa kwa miradi ya ULGSP kwa wakati
- Vielelezo mbalimbali kuhusiana na mradi wa ULGSP
- Watumishi waliohusika kwa namna moja au nyingine katika ucheleshwaji wa miradi na uthibitisho
- hali halisi ya fedha zilizopo
- Mapendekezo ya Miradi
- taarifa iandaliwe kwa siri

Vilevile taarifa hiyo itaonyesha yafuatayo:-

(i) MPANGO KAZI WA SHUGHULI ZA MRADI WA BENKI YA DUNIA

Kupitia mpango kazi wa shughuli zote za miradi ya ULGSP

(ii) MAPOKEZI YA FEDHA ZA ULGSP

Kupitia mapokezi ya fedha za mradi wa ULGSP kuanzia mwaka 2012/2013, 2013/2014, 2014/2015, 2015/2016 na vithibitisho vya mapokezi ya fedha hizo na kuanza kutumika

(iii) UTEKELEZAJI WA MATUMIZI YA FEDHA ZA ULGSP

- Kupitia taarifa za utekelezaji wa fedha za ULGSP
- Kupitia mchakato wa manunuzi kwa kila shughuli iliyotekelezwa
- Kupitia maombi ya vibali kutoka Taasisi mbalimbali ili kujiridhisha muda uliotumika tangu kuombwa kwa kibali husika hadi kutoka , pia kubaini taasisi iliyochelewesha maombi ya kibali cha kutekeleza shughuli hizo.

(iv) HATUA ZA HARAKA ZILIZOCHUKULIWA

Hatua za haraka zilizochukuliwa baada ya ucheleweshaji wa vibali

(v) KUBAINI WAHUSIKA WOTE WALIOSABABISHA KUCHELEWESHA KWA UKAMILISHAJI WA MIRADI HII

(vi) KUBAINI FEDHA ZILIZOPO MPAKA SASA NA KUTOA MAPENDEKEZO KWENYE BARAZA LA MADIWANI KUONYESHA NI MRADI GANI UTEKELEZWE KATIKA AWAMU YA PILI

(vii) REJEA MBALIMBALI

1. Mwongozo wa mradi wa ULGSP
2. Mpangokazi wa shughuli za ULGSP
3. Taarifa za utekelezaji wa shughuli za ULGSP
4. Bank statements kutoka akaunti ya mradi wa ULGSP
5. Risiti ya mapokezi ya fedha za ULGSP
6. Mikataba mbalimbali

7. Vielelezo mbalimbali/ barua Halmashauri ilikuwa inawasiliana na taasisi mbalimbali

8. Bajeti ya mradi

9. Mihtasari kuanzia mradi ulipoanza

Mwenyekiti alitaja kamati ndogo iliyofanya kazi kwamba ilihusisha wafuatao:-

1. Mhe. Alphonce Shushi Kulwa – Mwenyekiti
2. Bw. Immanuel S. Dyelu – Katibu
3. Mhe. Salum M. Lugembe - Mjumbe
4. Mhe.Hamida Omar Ally - Mjumbe
5. Mjumbe huyu alitakiwa kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Tabora

Aidha Mwenyekiti alitoa maelezo ya kina kwamba jumla ya nyaraka 44 kutoka Idara za fedha , MipangoMji, Utumishi na Utawala, Kitengo cha Ugavi, Mipango, Ujenzi na Usafi wa Mazingira zimepitiwa na kamati hii ambapo nyaraka hizo ni kama zifuatazo:- Mihtasari ya Baraza la Madiwani na Kamati ya Fedha na Uongozi, taarifa za kibenki (Benki Statement) kuanzia mwaka 2014/2015 hadi 2016/2017, taarifa ya utekelezaji wa mradi, Mpango kazi wa miaka 5 ya utekelezaji wa mradi, mwongozo wa mradi, mpango wa manunuzi wa mwaka 2015/2016 na 2016/2017, majalada ya Mikataba mbalimbali ya miradi, Ripoti za tathimini za tenda mbalimbali, Vitabu vya Bajeti, majalada ya vocha za mradi na majalada yaliyokuwa yakifanya mawasiliano na Taasisi mbalimbali kama vile Baraza la Hifadhi ya Mazingira ( NEMC) na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Baada ya kupitia nyaraka hizo kamati imebaini mambo mengi juu ya utekelezaji wa mradi huo ambayo yataelezwa kwenye taarifa hii. Pamoja na hilo pia Kamati ilipata muda wa kutembelea Kata 13 za Mjini ili kubaini matumizi ya fedha za kujenga uwezo na kutambulisha mradi huu ngazi ya Kata. Taarifa kwa kirefu itatolewa kwenye taarifa hii.

Sambamba na hilo kamati ilifanya mahojiano ya ana kwa ana na Mstahiki Meya wa Manispaa , Mkurugenzi wa Manispaa, Wakuu wa Idara za Mazingira , Mwanasheria , Mhandisi, Afisa Mipango Mij, Mkaguzi wa Ndani, Mchumi, Mweka Hazina, Afisa Utumishi na Afisa Manunuzi. Baada ya kuhojiana na Wakuu wa Idara, Kamati iliona kuwa bado inahitaji kujiridhisha zaidi na kuomba nyaraka za ziada na wahojiwa wa ziada walio chini ya Wakuu wa Idara za Manunuzi, Mhandisi na Utumishi na Utawala.

Kamati imejiridhisha katika maeneo mbalimbali ya utekelezaji wa mradi huu na kubaini kipi na nani aliyechangia kucheleweshа utekelezaji wa mradi huu pia kamati imebaini ubadhilifu wa matumizi ya fedha hizi ambao utatolewa ufafanuzi wa kina katika taarifa hii.

Sambamba na hili, pia kamati imebaini baadhi ya miradi ambayo imetekelezwa kwa wakati na kutokuwa na changamoto yoyote yenye madhara kwa mradi na Manispaa kwa ujumla.

Baada ya Kamati kupitia nyaraka zilizowasilishwa pia imebaini fedha zilizopokelewa na zilizotumika kuanzia mwaka 2014/2015 hadi mwaka 2016/2017 na imetoa mapendekezo yake juu ya utekelezaji wa miradi hii hadi kukamilika kwake.

Mwenyekiti alionyesha uchambuzi wa namna hadidu za rejea zilizofanyiwa kazi pamoja na Wataalamu waliohojiwa yakiwepo maelezo ya kila mtaalamu aliyehojiwa ambayo yalikua yamesainiwa na Wataalamu kukiri kwamba hayo ni maelezo yao sahihi

Vile vile kamati ilitoa ushauri kwenye Baraza la Madiwani kuhusiana na vipengele vyote muhimu ilivyokua imevifanyia kazi

Kamati pia ilibainisha wahusika wote waliosababisha kuchelewa kwa ukamilishaji wa miradi hii kama ifuatavyo

i. Mhandisi wa Ujenzi Manispaa Tabora
ii. Afisa Manunuzi wa Manispaa ya Tabora
iii. Mkurugenzi wa Manispaa ya Tabora
iv. Mstahiki Meya wa Manispaa ya Tabora

Kamati ilipendekeza Mradi unaotakiwa kutekelezwa katika awamu ya pili uwe ni mradi wa ujenzi wa soko la kisasa kutokana na Halmashauri kubaki na shs 8,997,104,844.04

Vile vile kamati ilipendekeza kufanyika kwa mafunzo ya Wahe Madiwani na Wataalamu juu ya kanuni na sheria mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya kila siku kwa muda wa siku 14(kumi na nne) kwa gharama ya Tshs 96,090,000/= (Millioni Tisini na sita na tisini elfu)

Baada ya taarifa hii kuwasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati, Mstahiki Meya aliwakaribisha Wajumbe kuijadili taarifa hii kwa kina ukurasa kwa ukurasa ili hatimaye waweze kuitolea maamuzi. Aidha Mstahiki Meya aliishauri Kamati ya Halmashauri kwamba kabla ya kuanza kuchangia Wataalamu waliohojiwa na Kamati

ya Uchunguzi waulizwe ili wakiri kama kweli maelezo yaliyotolewa na kamati yapo sahihi.

Waliohojiwa walikua kama ifuatavyo:-

**1.MSTAHIKI MEYA (Mhe. L.C. Ulaya ) Uk. wa 29**

Alieleza kwamba maelezo aliyotoa kwenye kamati ya uchunguzi ni kama yalivyo kwenye jedwali Na. 2 katika ukurasa wa nane (8) wa "TAARIFA YA KAMATI NDOGO YA UCHUNGUZI WA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MRADI WA BENKI YA DUNIA (ULGSP) KATIKA HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA," Kwamba siyo kweli kuwa kikao cha Kamati ya Fedha na Uongozi cha tarehe 29.04.2016 kiliazimia barabara ya Hill itolewe na isomeke barabara ya Rehani. Tatizo hilo kama lipo huenda lilikuwa ni kosa la uchapaji (Typing error) tu. Kwa kuthibitisha usemi huo, Mstahiki Meya aliikabidhi Kamati ya Uchunguzi Muhtasari wa kikao cha kamati ya Fedha wa tarehe 13 .01.2017 unaothibitisha kuwa barabara hiyo ya Hill ipo na wala haikuondolewa na Kamati ya Fedha katika kikao chake cha tarehe 29.4.2016

Aidha, Mstahiki Meya alishtushwa na taarifa hiyo kuonekana tena ukurasa wa 29 kwenye maelezo ya namba 3 ya TAARIFA HIYO YA KAMATI YA UCHUNGUZI, ikishutumu Kamati ya Fedha kwamba katika kikao chake cha 29.4.2016 iliazimia barabara ya Hill itolewe na isomeke barabara ya Rehani. Kamati ya Halmashauri ililiona jambo hili kuwa ni la kipotoshaji. Hivyo Kamati ya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ikaona kwamba Kamati ya Uchunguzi imetoa taarifa ambayo haina ukweli wowote, bali upotoshaji.

**(2)MKURUGENZI MANISPAA-UK 8. ( Bw. Bosco O. Ndunguru)**

Alisema kuhusu hoja aliyoulizwa kuhusu mkataba wa PUMA Logistics kwamba alijibu nitafuatilia. Lakini hakuridhika na maelezo yaliyokuwepo katika taarifa kwa kuwa mkataba huo ulipofuatiliwa ulikuwa umesainiwa na Mkurugenzi **Sipora .J. Liana,** kwa thamani ya Tshs 442,000,000/= Mkurugenzi alishangaa kuikuta Kamati ina Mkataba ambao haujasainiwa ukiwa na thamani Tshs 429,380,000/=. Hivyo maelezo yaliyotolewa kwenye taarifa ya Kamati ya Uchunguzi siyo sahihi aliomba masahihisho aliyoyatoa yafanyike.

Mkurugenzi vilevile alisema maelezo yaliyotolewa na Wasaidizi "Subordinates"wa Wakuu wa Idara yasingeandikwa badala yake yatumike maelezo yaliyotolewa na Wakuu wa Idara na vitengo.

Alisisitiza pia kwamba katika taarifa hiyo Kamati ilitakiwa kuonyesha ni Wataalamu gani wanatakiwa wachukuliwe hatua (kwa majina na vyeo vyao), kitu ambacho Kamati hiyo ya Uchunguzi haikufanya.

Mkurugenzi aliitaja Miradi iliyokuwa inatakiwa kuzungumziwa kwenye taarifa hiyo ni ujenzi wa soko la kisasa, Barabara na ujenzi wa stendi mpya. Aidha kuhusu ununuzi wa greda na gari la kubeba taka ngumu pamoja kontena zake alisema tayari mitambo hiyo ilishanunuliwa na hivyo kuwepo kwake katika taarifa hiyo siyo sababu ya kuchelewesha mradi.

(3)**MATHIASI LUKALA**- Kaimu Afisa manunuzi alikiri maelezo yake yapo sahihi.

(4)**MWANASHERIA**-(Theodora Chuwa) - Alikiri maelezo yake yapo sahihi

(5)**AFISA MPANGO MIJI** - (Bw. G.A. Mwakalukwa) Alikiri maelezo yake yapo sahihi

(6)**MWEKA HAZINA** - ( Bw. Abbas Mwangosi) Alikiri maelezo yake yapo sahihi

(7)**MKAGUZI WA NDANI** - (Bw. Josephat Lema) Alikiri maelezo yake yapo sahihi

(8)**MCHUMI MANISPAA** - (Bw. Johanes Kilonzo)Alikiri maelezo yake yapo sahihi

(9)**AFISA UTUMISHI** - (Bibi Getruda Gisema) Hakuwepo kikaoni

(10)**MHANDISI UJENZI** - ( Eng . leonidas Sospeter) Hakuwepo kikaoni

(11)**DEO MANAE** - Mhandisi Hakuwepo kikaoni

(12)**STEVEN WARIOBA** - (Ujenzi barabara)Alikiri maelezo yake yapo sahihi

(13)**GAITANI MKENGE** - (Fundi Mkuu) Alikiri maelezo yake yapo sahihi

(14)**AFISA UGAVI** - (D. G'holombi) Hakuwepo kikaoni

(15)**TULIZO KISUMO** -(Afisa utumishi) Hakuwepo kikaoni

UK 16 -Neno **ubadhilifu** litoke katika ukurasa huo kwenye eneo la Mkaguzi wa Ndani.

UK 18 - Chuo cha Uhazili isomeke Chuo cha **Utumishi wa Umma** katika ukurasa huu.

UK 29 - Kwenye maelezo namba 2 juu, sentensi isomeke kwamba Barabara za Lwanzari (0.34Km) na Rufita (0.63Km) hazijatolewa kwenye mpango na kupelekwa Tuwatugawe na Salmini.Taarifa iliyotolewa na Kamati ni upotoshaji kwani haikujiridhisha na usahihi wa taarifa ambazo zipo katika Idara ya Ujenzi.

Fedha Tshs **10,066,684,547.95** katika( ukurasa huu zisomeke **10,066,692,547.95** ndio takwimu sahihi ya fedha hizi

**UKURASA WA (40 - 41)** Mstahiki Meya Asihusishwe na tuhuma yoyote kwa kuwa yeye hahusiki kuruhusu greda kufanya kazi pamoja na kutokusimamia tenda ya ununuzi wa gari moja na kontena 20 kutokana na upungufu wa vifaa vyenye thamani ya Tshs 2,493,340/= kwani kazi hiyo siyo yake bali ni ya Mkurugenzi kwa kuwa huo ni utendaji. Pia kutoisimamia Halmashauri vizuri na kuiingizia hasara ya Tshs 335,920,000/= kwa kutomkata mzabuni gharama za usumbufu (liquidated Damage 0.20%). Hii siyo sahihi kwa sababu haiwezekani gari na kontena 20 linunuliwe Tshs 442,000,000/= halafu ikatwe " Liquidated damages" kiasi cha Tshs 335,920,000/= hapo mzabuni atakuwa amefanya biashara gani? Aidha suala la kukata "liquidated damages" ni la na hivyo halimhusu Mstahiki Meya. Mstahiki Meya asihusishwe na suala la kushindwa kusimamia kikamilifu majukumu yake ambayo yameainishwa kwenye kanuni za kudumu za Halmashauri. Kanuni na 42 (3) kifungu kidogo cha (xix) hadi (xx) kwa kuwa vifungu vyote hivi harimhusu na isitoshe haya yote yaliyotajwa hayahusiani na maagizo yaliyokuwa yametolewa na Baraza la Madiwani kufanyiwa kazi na Kamati Ndogo, hivyo Baraza la Madiwani lilimwondolea Mstahiki Meya tuhuma zote zilizo kuwa zimeainishwa kwenye ukurasa wa (40 -41).

**UAMUZI WA BARAZA LA MADIWANI BAADA YA KUREJEA KUTOKA KWENYE KAMATI YA MADIWANI**

Baada ya Mwenyekiti wa kamati ndogo kuhitimisha kujibu hoja za wajumbe na kufanyika masahihisho tajwa hapo juu, wajumbe wa Baraza la Madiwani walitoa uamuzi kwamba:-

Baraza la Madiwani lilimuona Mstahiki Meya hahusiki na tuhuma yoyote kama zilivyokuwa zimeainishwa na Kamati Ndogo iliyoteuliwa na Baraza la Madiwani tarehe 21/01/2017 kwenye ukurasa wa 40 (7.4) hadi uk 41. Aidha, kwa vile kamati hiyo Ndogo imeshindwa kubainisha na kutaja wazi ni sababu gani na ni nani waliosababisha kuchelewa kuanza kwa mradi wa Benki ya Dunia na hivyo Kamati hii iliyokuwa imeundwa na Baraza la Madiwani tarehe 21/1/2017 kushindwa kufanya kazi iliyotumwa na Baraza la Madiwani , Hivyo Baraza la Madiwani limeikataa taarifa hiyo.

Aidha Mkurugenzi Manispaa aendelee kufuatilia tuhuma zinazowahusu wataalamu ambao hawajatajwa wazi wazi kwenye taarifa hiyo ili kupata ukweli wake.

**MUHT: NA. MBM 4/2016/2017/6 KUAHIRISHA BARAZA LA MADIWANI SIKU YA KWANZA**

Mwenyekiti aliahirisha Mkutano siku ya kwanza tarehe 27/2/2017 saa 1.54 usiku

SIKU YA PILI TAREHE 28/2/2017.

Siku ya pili tarehe 28.2.2017 wajumbe waliendelea na baraza la madiwani kwa kujadili agenda zilizokuwa zimebakia kama ifuatavyo:-

MUHT: NA. MBM4/2016/2017/7 - KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA BARAZA LA MADIWANI LILILOFANYIKA TAREHE 11/11/2016 NA 12/11/2016:

Muhtasari huo ulisomwa mbele ya wajumbe wote na kuthibitishwa kuwa ni sahihi, hivyo Mwenyekiti aliusaini ili kuwa kumbukumbu sahihi ya Mkutano huu katika Halmashauri.

MUHT: NA. MBM4/2016/2017/8 - YATOKANAYO NA MUHTASARI WA TAREHE 11/11/2016 NA 12/11/2016:

Yatokanayo yaliwasilishwa pamoja na utekelezaji wake kama inavyoonekana hapa chini:-

**(1)BARAZA LILIAGIZA MKUTANO UJAO LIPATIWE MAJIBU YA HOJA ZA MADIWANI KUHUSU TAA ZA BARABARANI KUTOKANA NA KUTORIDHIKA NA MAJIBU YALIYOTOLEWA NA MENEJIMENTI KWENYE BARAZA LILILOPITA. HOJA HIZO NI KAMA IFUATAVYO:-**

(1) Taa za barabarani zinazohusu Halmashauri ya Manispaa. Mkakati wake wa kuziwasha muda wote ukoje, **utekelezaji** ilielezwa kuwa taa za barabarani zinazoihusu Halmashauri ya Manispaa zinasubiri OC itakapoingia ndio zishughulikiwe.

Taa za barabarani zinazomhusu Wakala wa barabara (TANROAD), Mkakati wake wa kuziwasha muda wote ukoje, **utekelezaji** ilielezwa kuwa taa za barabarani zinazomhusu Wakala wa barabara (TANROAD) kwa mujibu wa maelezo aliyoyatoa kwa mdomo toka kwa meneja ni kwamba atalipia bill ya mwezi mmoja na baada ya hapo atakabidhi taa hizo Manispaa. Hata hivyo barua Kumb. Na.TMC/WD/REB/VOL.II/87 ya tarehe 16.2.2017 kwenda kwa Wakala wa barabara (TANROAD) ilikwishaandikwa.

AZIMIO:

Baada ya kupokea na kujadili jibu hili la utekelezaji, wajumbe waliazimia kuwa ifanyike tathmini ya taa za barabarani na kikao kijacho cha kamati ya fedha kiwasilishiwe tathimini hiyo ikiwa na mpango na bajeti. Aidha kwa upande wa barabara za miradi ya benki ya dunia ilisisitizwa uwepo mpango maalumu wa taa za barabarani.utakaowaelekeza wakandarasi wanaojenga barabara hizo kuweka taa za barabarani.

**(2)MKUU WA MKOA TABORA AANDIKIWE BARUA YA PONGEZI KWA USIMAMIZI WAKE MADHUBUTI KATIKA BWAWA LA UMWAGILIAJI INALA. PONGEZI HIZI PIA ZIWALENGE WANANCHI WA KIJIJI CHA INALA KUPITIA MHE. DIWANI WA KATA YA NDEVELWA KWA USHIRIKI WAO MZURI TOKA MRADI HUU ULIPOANZA KUTEKELEZWA.**

Ilitolewa taarifa kwamba agizo hili lilitekelezwa kwa barua Kumb. Na.TMC/WD/R/VOLII/87 ya tarehe 30.12.2016 ambayo iliandikwa kwenda kwa Mkuu wa Mkoa kwa ajili ya kumpongeza.

**MSISITIZO WA WAJUMBE:**

Baada ya kupokea jibu hili wajumbe walisisitiza Mhe. Diwani wa Kata ya Ndevelwa aandikiwe barua ya pongezi kwa niaba ya wananchi wa Kata ya Ndevelwa kutokana na ushiriki wao mzuri toka mradi huu ulipoanza kutekelezwa.

**(3)WATENDAJI WA KATA AMBAO WALIKUWA BADO HAWAJAWASILISHA TAARIFA YA MADENI YA PANGO LA OFISI ZAO KWA MKURUGENZI, WAWASILISHE HARAKA ILI AANZE KUFANYIA KAZI:**

Ilitolewa taarifa kwamba watendaji wa Kata 9 wanaodaiwa pango waliwasilisha taarifa kwa Mkurugenzi. Taarifa hiyo ina jumla ya Tshs. 13,620,000/= tarehe 29.11.2016 suala hili liliwasilishwa Kamati ya Fedha ambapo waliridhia fedha hizo zilipwe na Halmashauri.

**AZIMIO:**

Baada ya kupokea na kujadii taarifa hii ya utekelezaji Baraza liliazima kuwa Halmashauri ilipe kodi ya pango kiasi cha Tshs. 13,620,000/= zinazodaiwa na kata 9, hivyo Baraza lilitoa muda wa mwezi mmoja kwa menejimenti kulipa deni hilo lapango la Ofisi za Watendaji Kata na taarifa iwasilishwe Kamati ya Fedha na Utawaa.

**(4)BARAZA LILITOA MUDA WA MIEZI 4 KUHAKIKISHA KAZI YA KUHAKIKI MIPAKA YA KATA MBALIMBALI ZENYE MIGOGORO NA JESHI INAKAMILIKA. AIDHA KATIKA ZOEZI HILI WASHIRIKISHWE WAHE. MADIWANI PAMOJA NA VIONGOZI WENGINE NDANI YA KATA:**

Ilitolewa taarifa kwamba mpaka na Jeshi Kata ya Mbugani na Misha ulihakikiwa na kufufua alama za upimaji, zoezi litaendelea kwa Kata za Mtendeni, Kitete, Cheyo, Kalunde wa Tumbi kwa kipindi cha Julai - Oktoba 2017.

**(5)MENEJIMENTI IMWANDIKIE BARUA MWENYEKITI WA MTAA WA IKINDWA KUMJULISHA KWAMBA MTAA ANAOUONGOZA UKO KATA YA MAPAMBANO, HIVYO ANATAKIWA KUHUDHURIA VIKAO VYA WDC KATA YA MAPAMBANO:**

Ilitolewa taarifa kwamba barua Kumb. Na. TMC/U/72/181 ya tarehe 29.12.2016 iliandikwa kwa Mtendaji wa Kata ya Mapambano kumjulisha kuwa mtaa wa Ikindwa upo Kata ya Mapambano kiutawala. Nakala ya barua hiyo alipewa Mwenyekiti wa Mtaa wa Ikindwa.

**UAMUZI WA BARAZA LA MADIWANI JUU YA MTAA WA IKINDWA:**

Baada ya kujadili kwa kina jibu la utekelezjai lililotolewa na menejimenti Baraza la Madiwani lilibaini kwamba Mtaa wa IKINDWA upo Kata ya Mtendeni, hivyo liliagiza kufutwa kwa barua Kumb. Na.TMC/U/72/181 ya tarehe 29.12.2016 ambayo aliandikiwa Mtendaji wa Kata ya Mapambano na nakala kupewa Mwenyekiti wa Mtaa wa Ikindwa, sababu ya kuifuta barua hiyo ni kwamba Halmashauri ya Manispaa Tabora iliandika barua hiyo kabla ya Waziri mwenye dhamana hajatoa maamuzi yake.

Hivyo Baraza liliagiza Kamati za Maendeleo za Kata ya Mapambano na Mtendeni zikae pamoja kulijadili suala hili na makubaliano yatakayofikiwa yawasilishwe Baraza la Madiwani lijalo. Aidha Idara ya Mipangomiji ionyeshe haraka mipaka ya Kata ya Mapambano na Mtendeni ili ijulikane.

**(6)BARAZA LILIAGIZA ZITOLEWE SH. 5,000,000/= KWA AJILI YA KUCHIMBUA NA KUSAFISHA MFEREJI WA KILIMBIKA ULIOPO KATA YA ISEVYA ILI KUZUIA MAFURIKO WAKATI WA MASIKA:**

Ilitolewa taarifa kwamba fedha Tshs. 5,000,000/= zilishatolewa na kupelekwa WDC Kata ya Isevya kwa ajili ya kazi iliyotajwa hapo juu.

**PONGEZI:**

Baada ya Baraza la Madiwani kuipokea taarifa hii liliipongeza menejimenti kwa kutekeleza mapema agizo la Baraza la Madiwani.

**(7)MENEJIMENTI IHARAKISHE KUFANYIA KAZI MCHAKATO WA SOKO LA T/RELI ILI PAGAWANYWE SEHEMU YA SOKO NA SEHEMU YA MICHEZO:**

Ilitolewa taarifa kwamba bango la kuwatangazia wananchi kutoa maoni juu ya kusudio la kugawanya eneo hilo la wazi liliwekwa tarehe 28.12.2016 na mapendekezo yaliwasilishwa Kamati ya Mipango miji na Mazingira tarehe 14.2.2017.

PONGEZI:

Baada ya kupokea jibu la utekelezaji huu wajumbe waliipongeza menejimenti kwa kutekeleza agizo hili la Baraza la Madiwani. Aidha walisisitiza menejimenti ilifanyie kazi haraka suala hili ili paweze kugawanywa eneo la soko, kiwanja cha kujenga ofisi ya Kata na kubakiza eneo la wazi kwa ajili ya huduma mbalimbali.

(8)UCHUNGUZI UFANYIKE KATIKA SHULE YA SEKONDARI RWANZARI KUONA WANANCHI WALIOJENGA KATIKA ENEO HILO KAMA WALIVAMIA AU WALIGAWIWA ILI HATUA ZICHUKULIWE KWA WALIOHUSIKA.

Ilitolewa taarifa kwamba jumla ya wananchi 6 walionekana kuvamia eneo hilo la shule, aidha hakuna vibali vya umiliki kutoka Manispaa na hata vibali vya ujenzi, zoezi la kuwaondoa litafanyika.

AZIMIO:

Baada ya kupokea jibu la utekelezaji huu wajumbe waliazimia kuwa ili kulipatia ufumbuzi suala hili Kata ya Ng'ambo na Gongoni zikutane kulifanyia kazi suala hili, Aidha idara ya Mipangomiji ishiriki katika kikao hicho wakiwepo na wananchi wa eneo hilo.

(9)MENEJIMENTI IREJESHE 20% IKIWA NI "SERVICE LEVY" YA FEDHA TSHS. 187,959,314.92 KWENYE KATA ZOTE KULIKOFANYIKA UJENZI WA BARABARA ZA LAMI:

Ilitolewa taarifa kwamba fedha hizi zilipokelewa na Halmashauri kwa vipindi tofauti katika mwaka wa fedha uliopita 2015/2016 na zilitumika kwa shughuli za maendeleo kwa kufuata bajeti pamoja na maagizo ya viongozi ya utengenezaji wa madawati na ujenzi wa maabara katika shule zetu kwa Kata zote.

(10)MENEJIMENTI IWASILISHE KAMATI YA FEDHA TAARIFA KUONYESHA MCHANGANUO WA VYANZO VYA MAPATO KWAMBA KWA MWAKA 2015/2016 KILA CHANZO CHA MAPATO KILITUINGIZIA KIASI GANI CHA FEDHA:

Ilitolewa taarifa kwamba taarifa hii iliwaislishwa kwenye kikao cha Kamati ya Fedha na Utawala tarehe 13.1.2017 ambapo Kamati iliagiza ipangiwe siku maalumu ili ikafanye uhakiki.

AZIMIO:

Baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji huu wajumbe waliazimia kwamba ili kupata takwimu sahihi ya vyanzo vyetu vya mapato kila kata ihakiki vyanzo vyake vya mapato vilivyo ndani ya Kata yake baada ya kukamilika zoezi hilo taarifa hiyo iwasilishwe kwa Mkurugenzi ambaye naye ataiwasilisha Kamati ya Fedha na Baraza la Madiwani, lijalo.

(11)FEDHA TSHS. 12,377,034.71 ZA UJENZI WA BELLING SHED KIJIJI CHA IGOMBE KWA KUWA SUALA LAKE LILISHAPELEKWA POLISI, TAARIFA YA HATUA ILIYOKWISHAFIKIWA IWASILISHWE KAMATI YA FEDHA:

Ilitolewa taarifa kwamba Ofisi ilifuatilia suala hili polisi na kupewa taarifa kwamba upelelezi umekamilika na jalada la kesi hii limepelekwa kwa Mwanasheria wa Serikali ili aweze kutoa maamuzi kama kesi hii ipelekwe Mahakamani au la. Watumishi 2 kati ya watatu walikamatwa na kushikiliwa na polisi lakini wapo nje kwa dhamana. Tunaendelea kufatilia suala hili ili liweze kufikishwa mahakamani.

MSISITIO WA WAJUMBE:

Baada ya kupokea jibu hili la utekelezaji wajumbe walisisitiza menejimenti iendelee kufuatilia suala hili .

(12)ILIAGIZWA MKURUGENZI AIAGIZE MAMLAKA YA NIDHAMU (TSC) KUWACHUKULIA HATUA WALIMU WAKUU WALIOSABABISHA WANAFUNZI HEWA PAMOJA NA KUHAKIKISHA WANAREJESHA FEDHA. SHULE HIZO N I KAKOLA, MAGOWEKO, IZENGA NA UHURU:

Ilitolewa taarifa kwamba hatua zilichukuliwa kwa Walimu Wakuu wanne (4) wa shule tajwa hapo juu kwa kuwasimamisha kazi kwa ajili ya uchunguzi. Barua Kumb. Na.TMC/AEM/170/VOL.III/46 ya tarehe 20.11.2016 yahusika.

PONGEZI:

Baada ya kujadili Baraza liliipongeza menejimenti kwa utekelezaji wa agizo hili.

(13)MENEJIMENTI IFANYE MANUNUZI YA MITAMBO NA GREDA NA KUHAKIKISHA IFIKAPO TAREHE 30.1.2017 UWE IMEFIKA KATIKA HALMASHAURI YETU:

Ilitolewa taarifa kuwa mtambo wa greda umeshawasilishwa na mzabuni hapo tarehe 1/12/2016 ulikaguliwa na kupokelewa na wataalamu/wakaguzi na unetolewa kwa Idara ya Ujenzi kwa matumizi.

(14)BARAZA LIJALO LIPATIWE TAARIFA YA KUUNGUA MOTO OFISI YA UCHAGUZI ILI WAHE. MADIWANI WAFAHAMU HATUA ILIOFIKIWA:

Mkurugenzi alilifahamisha Baraza la Madiwani kwamba suala hili bado lipo kwenye hatua ya uchunguzi wa vyombo vya dola, hivyo mpaka sasa hajaletewa taarifa yeyote juu ya suala hili.

MAJADILIANO YA WAJUMBE JUU YA HOJA HII:

(1)**Mhe Hamida Ally - Diwani Viti Maalumu.** Alilifahamisha Baraza la Madiwani kwamba azimio hili limekosewa lilikuwa linahusu Baraza la Madiwani kupatiwa taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za uchaguzi ambapo ilitakiwa taarifa hii iwasilishwe na Mkaguzi wa Ndani Manispaa.

MAJIBU YA MKURUGENZI :

Alisisitiza jibu lake alilolitoa hapo juu kwamba taarifa hiyo bado hatujaletewa hapa Halmashauri na vyombo vianvyolifanyia kazi suala hili.

(2) **Mhe: Rehema Kabata - Diwani Kata ya Chemchem.** Alisema tulitaka Mkaguzi wa Ndani atoe taarifa hiyo, hatutaki suala la uchunguzi toka polisi

MAJIBU YA AFISA UCHAGUZI:

Alisema baada ya Ofisi kuungua moto tulitoa taarifa polisi na tume ya ucahguzi ambayo ilihitaji taarifa hiyo.

USHAURI WA MKURUGENZI:

Aliwashauri wajumbe kwamba vitu ambavyo vipo nje ya uwezo wa ofisi yake, wajumbe wawe wavumilivu kwani suala hilo lipo nje ya uwezo wa Mkurugenzi, kwa kuwa taarifa wanayohitaji wahe. Madiwani hana.

(3) **Mhe: Shushi Kulwa - diwani Kata ya Itonjanda.** Alisema jambo hili lina masuala mawili (2):

(i) Baraza la mwezi wa tano liliagiza Mkaguzi wa Ndani akakague taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za uchaguzi.

(ii)Tarehe 2.6.2016 ofisi hiyo ya Uchaguzi ikaungua moto, alihoji kwa nini ofisi iliungua baada ya azimio la madiwani kutoka .

**(4)MHE. SALIMU MSAMAZI - DIWANI KATA YA IKOMWA:**

Alisema katika muhtasari wa Kamati ya fedha wa tartehe 29.6.2016 ukurasa wa 5, inaonyesha jumla ya Tshs. 5,000,000/= zilirudishwa Tume ya Uchaguzi. Alisisitiza mkaguzi wa ndani alete taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za uchaguzi ili tufunge hoja hii, Aidha alisisitiza kwamba Mkurugenzi atueleze kama Baraza halina uwezo kusimamia ofisi ikiungua moto katika mazingira tata.

**Majibu ya Mkurugenzi:**

Baraza hili linaongozwa kwa kanuni na sheria, alishauri azimio hili litenguliwe kwa kuwa muda wa miezi 6 umefika, toka azimio hili litolewe.

(5)**Mhe. Yasini Kushoka - Diwani Kata ya Misha:**

Alisema hili suala la uchaguzi tulishalizungumza na tulishaelezwa fedha hizo zinahusika na Tume ya uchaguzi - alisisitiza suala hili tulitoe kwani limekuwa la muda mrefu.

(6)**Mhe. Kapela Ramadhani Shabani - Diwani Kata ya Isevya:**

Alisema Mkaguzi wa Ndani alishalieleza Baraza la Madiwani kwamba Halmashauri haihusiki na fedha za uchaguzi; vile vile alilieleza Baraza la Madiwani kwamba Mhe. Msamazi alimtaka Frenki ampe fedha vinginevyo atamng'oa.

(7)**Mhe. Paulo Kananda - Diwani Kata ya Mbugani**

Aliwaomba Wahe. Madiwani wawe watulivu, alisema tukubali vyombo vilifanyie kazi suala hili, sisi Wahe. Madiwani hatuwezi kubaini mpaka vyombo vituletee. Aliomba hoja hii iondolewe kwa kuwa tunaingilia muhimili mwingine, tufuate kanuni, taratibu na sheria (alisisitiza azimio hili lifutwe.

(8)**Mhe. Lucas Ndelemba - Diwani Kata ya Tumbi**

Alisema tunapokuwa na mjadala, mjumbe akatuhumiwa nini mwongozo wako Mwenyekiti.

MAJIBU YA MKURUGENZI

Alisema suala hilo itabidi wahusika watoe maelezo juu ya tuhuma hizi ambao ni Mhe. Kapela Ramadhani Diwani Kata ya Isevya, Frank Mkoga(Afisa Uchaguzi) na Mhe. Salum Msamazi Diwani - Kata ya Ikomwa.

UAMUZI WA BARAZA LA MADIWANI JUU YA AZIMIO HILO

Mwenyekiti ambaye ni Mstahiki Meya alilieleza baraza la madiwani kwamba kwa mujibu wa majadiliano tuliyofikia azimio hilo kwa sasa limeahirishwa mpaka pale taarifa ya uchunguzi kutoka Polisi itakapowasilishwa, Aidha baraza linatoa siku saba (7) kwa Mhe. Kapela Ramadhani Diwani Kata ya Isevya Bw. Frank Mkoga Afisa Uchaguzi na Mhe, Salum Msamazi - diwani Kata ya Ikomwa kutoa maelezo kuhusiana na tuhuma iliyotolewa na Mhe. Kapela Ramadhani kwamba Mhe. Salum Msamazi analifuatilia suala la kuungua moto Ofisi ya Uchaguzi kwa kuwa Bw. Frank Mkoga aliombwa hela na Mhe. Salum Msamazi, Alisema maelezo hayo yaanze kutolewa leo tarehe 28/2/2017 -7/3/2017 na kukabidhiwa kwa Mstahiki Meya mwisho wa kukabidhi ni saa 8 mchana ya tarehe 07/03/2017.

**(9) BARAZA LIJALO IWASILISHWE TAARIFA YA UKAGUZI MAALUM ULIOFANYIKA KWENYE IDARA YA MPANGO MIJI KUHUSIANA NA FEDHA TSHS 879,356,761.57 ILIYOKUWA IMEKUSANYWA KWA AJILI YA KULIPIA FIDIA TSHS 552,223,771 AMBAPO BAADA YA MALIPO HAYO ZILIBAKI TSHS 327,132,989.99**

Ilitolewa taarifa kwamba ukaguzi huo bado unaendelea, Taarifa kamili itawasilishwa baraza la madiwani lijalo

**(10)ILIAGIZWA UCHUNGUZI UFANYIKE KWENYE MAENEO YALIYOJENGWA KIHOLELA HUSUSANI KIWANJA CHA TBC NA MAENEO MENGINE ILI WALE WALIOHUSIKA AU KUSABABISHA UJENZI HUO WABAINISHWE**

Ilitolewa taarifa kwamba uchunguzi umefanyika hakuna mwananchi yeyote aliyekuwa na hati ya kumiliki kiwanja ndani ya eneo la TBC walio na kibali cha ujenzi. Hivyo wananchi hawa walivamia

**(11) LINI POSHO WANAYODAI WATENDAJI WA KATA YA BARAZA LA MADIWANI LA TAREHE 25/8/2016 WATALIPWA ILI KUWAONDOLEA USUMBUFU WA KUFUATILIA MADAI HAYO**

Ilitolewa taarifa kwamba posho inayodaiwa imeandaliwa na ipo tayari kulipwa kwa wahusika.

**AZIMIO**

Baada ya kupokea taarifa hiyo ya utekelezaji wajumbe waliagiza posho hiyo ilipwe haraka ndani ya siku tatu na taarifa iwasilishwe kamati ya fedha

**(12) MENEJIMENTI ILIFANYIE KAZI SUALA LA KUHAMISHA WALIMU ILI IKAMA YA WALIMU KATIKA SHULE ZOTE ZA MSINGI ILINGANE KWA KUZINGATIA KUWA KATIKA BAJETI YA 2016/2017 KIFUNGU KIPO KINA FEDHA UPANDE WA MOVING EXPENSE TSHS 9,366,000/=**

Ilitolewa taarifa kwamba fedha kwa ajili ya kurekebisha ikama ya walimu bado haijapatikana, Aidha tshs 9,366,000/= ni fedha ambayo ilishapokelewa na kutumika kulipia walimu wastafu stahili zao za usafiri na mizigo

**MSISISTIZO WA WAJUMBE**

Baada ya baraza kupokea jibu la utekelezaji huu lisisitiza suala hili la uhamisho litengewe fedha katika bajeti ya 2017/2018, Aidha Menejimenti kwa sasa ifanye uhamisho wa walimu wa ndani ili kuweka sawa ikama kwa shule zilizopo mjini.

**(13)MENEJIMENTI IWASILISHE KAMATI YA FEDHA ORODHA YA MAPATO YANAYOITAJIKA KWENDA KUCHUKULIWA TRA ILI WAHE MADIWANI WAFAHAMU KWA KUZINGATIA CHANGAMOTO HII IMEKUWA IKIJITOKEZA MARA KWA MARA KATIKA TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI**

Ilitolewa taarifa kwamba orodha ya wafanya biashara iliyokuwa imeombwa toka TRA imeshapatikana

**AZIMIO**

Baada ya kupokea na kujadili utekelezaji tajwa hapo juu wajumbe waliazimia kuwa orodha ya mapato yanayohitajika kwenda kuchukuliwa TRA iwasilishwe kamati ya fedha na baraza la madiwani lijalo kwa kuwa tayari orodha hiyo imepatikana.

**(14) BARAZA LIJALO LIWASILISHIWE TAARIFA KUONYESHA MPAKA SASA KUNA VIKUNDI VINGAPI VYA WANAWAKE NA VIJANA AMBAVYO VIMEKOPESHWA MIKOPO , NI SAWA NA ASILIMIA NGAPI KUTOKANA NA ASILIMIA KUMI (10) YA MAPATO YANAYOKUSANYWA NA HALMASHAURI**

Ilitolewa taarifa kwamba vikundi vya wanawake 19 na vijana 8 vilikopeshwa jumla ya Tshs 20,500,000/= kwa kipindi cha Julai - Desemba 2016 ambapo 10,500,000/= zimekopeshwa kwa vikundi vya wanawake na Tshs 10,000,000/= zimekopeshwa kwa vikundi vya vijana ambazo ni mchango wa Halmashauri wa 10% ya mapato ya ndani ikiwa ni sawa na 15.98% ya mapato ya ndani ambayo ni Tshs 62,581,580.76

**MSISISTIZO WA WAJUMBE**

Baada ya kupokea jibu la utekelezaji tajwa hapo juu wajumbe walisisitiza yafuatayo:-

(i) Uandaliwe mpango wa vikundi vitakavyopewa mikopo kwa dhana shirikishi, Aidha wahe madiwani na kamati za maendeleo za Kata (WDC) kwa ujumla wake zishirikishwe , Hali hii itawasaidia kutotoa mikopo kwa vikundi ambavyo haviko katika Kata husika na hivyo kutostahili kupewa mkopo ,pia ushirikishwaji huo utarahisisha ufuatiliaji na urejeshaji wa mkopo .

(ii) Menejimenti iandae taarifa inayoonyesha vikundi vilivyokopeshwa na vikundi ambavyo bado vinadaiwa. Pia kila kikundi kionyeshwe kinatoka Kata ipi

MUHT: NA. MBM 4/2016/2017/9 TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KUISHIA MWEZI DESEMBA 2016

Taarifa hii iliwasilishwa kwa wajumbe na kujadiliwa ambapo waliipokea na kusisitiza kwamba juhudi za makusanyo ya mapato ziongezwe kutokana na kwamba hadi mwezi Desemba 2016 Halmashauri ilikuwa imekusanya 34% tu, ambacho ni kiwango kidogo sana ya lengo la mwaka ambapo tulitakiwa kuwa na 50% hadi kufikia Desemba 2016. Aidha maazimo ya Kamati ya fedha na utawala ya tarehe 18/2/2017 yazingatiwe. Vilevile Menejimenti ifanyie kazi changamoto ilizoainisha kwenye taarifa sambamba na kufanyia kazi mikakati iliyoibuliwa ili kuongeza mapato ya Halmashauri. Pia uwepo nidhamu ya usimamizi wa mapato na matumizi ya mapato yote katika Halmashauri.

MUHT: NA. MBM 4/2016/2017/10 TAARIFA YA MKAGUZI WA NDANI ROBO YA PILI OKTOBA - DESEMBA 2016

Taarifa hii iliwasilishwa na kujadiliwa na wajumbe ambapo walimpongeza Mkaguzi wa ndani kwa kufanya kazi nzuri ya kuibua hoja mbalimbali kwa lengo la kuielekeza Menejimenti ifanye vizuri katika kuiendesha Halmashauri ili tusipate hati chafu. baraza pia liliunga mkono maoni yote yaliyotolewa na kamati ya fedha na utawala

MUHT: NA. MBM 4/2016/2017/11 KUPOKEA NA KUJADILI MIHTASARI YA KAMATI ZA KUDUMU:

Wajumbe walipokea na kupitisha mihtasari ya Kamati za Kudumu baada ya kuwasilishwa na wenyeviti wa Kamati za kudumu kama ifuatavyo:-

(1) KAMATI YA UKIMWI WA TAREHE 28/10/2016

Mwenyekiti aliwasilisha muhtasari huu na kupokelewa.

(2) KAMATI YA MIPANGO MIJI NA MAZINGIRA WA TAREHE 31/10/2016

Mwenyekiti aliwasilisha muhtasari huu na kupokelewa

(3) KAMATI YA UCHUMI, ELIMU NA AFYA WA TAREHE 1/11/2016

Mwenyekiti aliwasilisha muhtasari huu na kupokelewa

(4) KAMATI YA FEDHA NA UTAWALA YA TAREHE 2/11/2016 , 29/11/2016, NA 13/1/2017

Mwenyekiti aliwasilisha mihtasari hii na kupokelewa

MUHT: NA. MBM 4/2016/2017/12KUPOKEA NA KUPITISHA MAAZIMIO YA KAMATI ZA KUDUMU

Wenyeviti wa Kamati waliwasilisha maazimio haya kwenye baraza la madiwani na kupitishwa kamati ifuatavyo:-

(1) KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI YA TAREHE 13/2/2017

(i) Uhamasishaji kwa wazazi kuhusu kuwaelimisha watoto wao jinsi ya kujikinga na maambukizi ya Ukimwi uendelee. Hii ikiwa ni pamoja na kuwataka wazazi wa kiume na wa kike kuwa pamoja katika kuwaasa watoto wao

(ii) Watu waendelee kuelimishwa ili waepukane na imani potofu kwamba mtu anaweza kupona ukimwi baada ya kuombewa na wahubiri wa dini

(iii) Yatengenezwe mahusianao mazuri na ya karibu zaidi baina ya washauri nasaha na wanaokutwa wameambukizwa ukimwi.

(iv) Watu wanaopimwa na wasikutwe na virusi vya Ukimwi washauriwe watumie kondomu kwa sababu inawezekana wadudu wa HIV wamo lakini hawajaanza kuonekana

(v) Wateja wakitoa namba zao za simu wataalamu wazibipu papo hapo kwa sababu baadhi ya wateja hawatoi namba sahihi.

(vi) Watu ambao wamepimwa na kukutwa hawana ukimwi lakini wenzi wao (wapenzi wao) wamekutwa wameambukizwa wapelekwe kwenye vipimo vya juu zaidi. sababu ya kufanya hivyo ni kwamba watu hao wanaweza kuwa " carrier" na wakiachwa wanaweza kuambukiza watu wengi zaidi.

(2)KAMATI YA MIPANGO MIJI UJENZI NA MAZINGIRA YA TAREHE 14/2/2017

(1)Kuhusu suala la kudhibiti ujenzi holela ilipendekezwa kwamba:-

(i) Halmashauri itafute fedha za dharula kwa ajili ya kupima maeneo yote ambayo hayajapimwa na kuwekewa alama, hivyo wananchi watakaovamia maeneo yaliyopimwa wachukuliwe hatua ya kuvunjiwa.

(ii) Halmashauri ishirikishe wadau au Kampuni binafsi ili zisaidie kupima maeneo mbalimbali ambapo baadaye wananchi watauziwa na Halmashauri itapata mapato

(iii) Halmashauri iwasiliane na kamati mbalimbali za urasimishaji maeneo ambazo zimekuwa zikiundwa na Viongozi wetu (Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa) ili kukaa nazo na kuona ni namna gani tutalipa fidia na kuondoa migogoro ambayo baadaye husababisha uvamizi wa maeneo.

(iv) Kamati ya Mipango Miji na Mazingira ipatiwe mafunzo ili kuwajengea uwezo juu ya masuala ya kusimamia miundo mbinu mbalimbali katika Halmashauri yetu.

(2)Menejimenti iwasilishe taarifa ya magari mabovu yaliyopo Karakana ya Halmashauri ambayo yanatakiwa kuuzwa kutokana na uchakavu na mengine hayatengenezeki hususani magari na mitambo ili Kamati itoe mapendekezo yake kwenye baraza la Madiwani.

(3)Kutokana na kata za Kalunde , Mbugani, Mapambano na Kiloleni kuendelea kuwa na migogoro ya mipaka ziara ijayo kamati itembelee Kata hizo ili kwenda kuona mipaka inayogombaniwa na Kata hizo.

(4)kamati iliridhia ombi la kuligawanya eneo la wazi T/reli kama ifuatavyo:-

- Mita za mraba 3200 ziwe kwa ajili ya soko
- Mita 4450 ziendelee kutumika kama eneo la wazi la kupumzikia

(5)kuhusu suala la mgogoro wa uvamizi wa wananchi katika eneo la shule ya sekondari Rwanzari, kamati ilipendekeza kata ya Ng'ambo na kata ya Gongoni zikutane pamoja ili kulipatia ufumbuzi suala hili.

(6)Halmashauri irejeshe mifuko ya simenti ilizokopesha kata zilizokuwa zimetolewa na National Housing Corporation (NHC) kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.

(7)Menejimenti iwasilishe kamati ya Chama mchanganuo wa matengenezo ya magari kwa kuonyesha kila kifaa kilichonunuliwa na bei yake, hususani kwenye taarifa ya kitengo cha Karakana.

(8)Kuhusu suala la " Car wash" iliazimiwa kuwa mpaka kufikia tarehe 28/2/2017 Car wash zote zitakazokuwa zimekidhi sifa ziwe zimekata leseni, Aidha zile ambazo zitakuwa hazijakidhi sifa zinazotakiwa zifungwe.

(9)kwa upande wa taarifa ya maliasili ilisisitizwa orodha ya wafugaji wa nyuki kwa kila Kata iwe inaonyeshwa ili wahe. Madiwani waweze kufuatilia.

(10)Kwa upande wa barabara ya kutoka msalabani kupitia Kijiji cha Itaga hadi bwawa la Igombe imetelekezwa muda mrefu bila kutengenezwa, Hivyo kutokana na umuhimu wake kamati ilishauri ifanyiwe utaratibu ili itengenezwe.

(11)Kuhusu ombi la kukigawa kiwanja Na. 42 kitalu "A' Jamhuri kutokana na mgogoro wa umiliki wa kiwanja hicho baina ya wadhamini wa Chama cha mapinduzi na

Shirika la utangazaji la Taifa (TBC) inapendekezwa kuwa kiwanja hicho kibaki na kumilikiwa na wadhamini wa Chama cha Mapinduzi (CCM)

MAAMUZI YA NYONGEZA TOKA KWENYE BARAZA LA MADIWANI

1) Mkandarasi anayejenga mfereji wa Kata ya Mpela aelekezwe na Menejimenti avunje ili ajenge upya kutokana na mfereji huo kujengwa chini ya kiwango

2) Mfereji wa maji ya mvua uliopo Ulyankulu Road kuunga daraja linaloelekea Irewe mpaka Istiqama utengenezwe ili kudhibiti maji yanayozagaa kwa kukosa miundo mbinu mizuri ya mfereji huo.

(3)KAMATI YA UCHUMI, ELIMU NA AFYA YA TAREHE 20/2/2017

(i) Menejimenti ilifanyie kazi suala la Ikama ya walimu katika shule za misingi ili uwiano ulingane katika shule za Mjini na zilizo nje ya Mji, kwa kuwasilisha mapendekezo ambayo yatapelekwa kwenye Baraza la Madiwani kuonyesha sehemu ambapo fedha za kugharamia uhamisho wa Walimu zitaazimwa. Mapendekezo hayo yaambatane na taarifa ambayo itachanganua kila kitu kwa mfano posho ya kujikimu posho ya usumbufu nk.

(ii) Choo cha shule ya Msingi Kipera ( Matundu 18) kikamilishwe haraka

(iii) Uwanja wa vita uwe ni miongoni mwa vyanzo vya mapato na utolewe taarifa ya Mapato kila robo kama vyanzo vingine vya mapato vinavyotolewa taarifa .

(iv) Zichukuliwe hatua za haraka ili kujua taratibu zinazotumika katika ununuaji wa samani za vyumba vya madarasa ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika shule za Msingi Mwenge, Town School na Ipuli.

(v) Miradi inapopokelewa kwenye Kata taarifa na elimu vitangulie kwanza kabla ya utekelezaji wa miradi kuanza. Aidha pawepo na ushirikishwaji wa wahe. Madiwani pamoja na wadau wote wa miradi husika, sambamba na kufanya vikao vya "Site meeting" vikihusisha wadau wote kwa kila hatua.

(vi) Kuhusu fedha za ufuatiliaji ngazi ya kata zinazohusu shughuli za TASAF, wajumbe waliagiza kwamba iwasilishwe taarifa kwenye kikao cha Kamati ya Chama 25/2/2017, kuonyesha mchanganuo halisi wa fedha zilizopelekwa kwenye kila kata na kiwango chake pia pesa zilizopelekwa kwenye kila Kijiji ama Mtaa na Kiwango chake.

(vii) Mifugo inayozagaa ovyo Mitaani ikamatwe na kila mfugo (Ngombe) alipiwe faini ya shilingi elfu hamsini (Tshs 50,000). Ngombe ambao watakuwa

hawajalipiwa faini watapelekwa machinjioni ili kusubiri wenye mali wazifuate na kulipia faini

(viii) Taratibu zifanyike ili pesa shilingi milioni kumi (Tshs 10,000,000) zilizokuwa zimepelekwa shule ya Msingi Kiloleni iliyopo katika Kata ya Mapambano kwa ajili ya Ukarabati wa shule hiyo, lakini baadaye zikahamishwa na kupelekwa kwenye matengenezo ya soko lililopo Kata ya Kiloleni zirudishwe katika shule ya msingi Kiloleni .

(4)KAMATI YA FEDHA NA UTAWALA YA TAREHE 18/2/2017

1. Jitihada za haraka zifanyike ili bomba la maji Mtaa wa Ikulu Kata ya Cheyo lililopita kwenye nyumba namba 113 litolewe nje ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea iwapo litaendelea kubaki ndani ya nyumba hiyo.
2. Mhe. Mbunge apewe nakala ya barua zilizotumwa Wizara ya Kilimo , Mifugo na Uvuvi kwa ajili ya kuomba kuhamishwa mnada wa Ipuli kwa kuwa kwa sasa upo katikati ya Mji ili aweze kufuatilia
3. Taarifa ya 10% ya mapato yanayotakiwa kupelekwa kuchangia mfuko wa akina mama na vijana itolewe kwenye Kamati kila kikao. Aidha suala hili liende sambamba na kuonyesha vikundi vilivyokopeshwa na kiasi kilichokopeshwa kwa kila kikundi.
4. Kwa upande wa mikakati mipya ya kuongeza vyanzo vya mapato ziandaliwe Sheria ndogo (By Laws) kwa ajili ya kukusanya vyanzo vipya vinavyoibuliwa na Halmashauri.
5. Wenye malori makubwa ambao hawaendi kuegesha kwenye maegesho ya malori Ipuli wapigwe faini ya Tshs 50,000/= ili kuwalazimisha kwenda kwenye eneo letu la Ipuli. vilevile wasimamie vizuri zoezi hili kwani kuna baadhi ya magari hayalipi mapato ya maegesho kwa kuwa wakusanyaji mapato hawafiki baadhi ya maeneo na kuikosesha Halmashauri mapato.
6. Menejimenti ilifanyie kazi haraka suala la vitambulisho vya wahe. Madiwani
7. Suala linalofanywa na Mkoa kupitia Katibu Tawala Mkoa, kuja Halmashauri ya Manispaa Tabora na kuagiza watumishi kadhaa kusimamishwa kazi bila wahe.Madiwani kupewa taarifa lifikishwe baraza la madiwani tarehe 28/2/2017 ili lijadiliwe na kutolewa Tamko
8. kamati iliipongeza menejimenti kwa kuendesha mafunzo kwa kada ya maafisa utumishi na waandishi wa vikao yaliyofanyika Mwanza kwani yataleta ufanisi

wa kazi kwa kuzingatia kuwa mafunzo hayo yalipitishwa kwenye bajeti yetu ya mwaka 2015/2016 ili kuwajengea uwezo.

9. Kikao kijacho menejimenti iwasilishe BOQ za ujenzi wa madarasa kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu yanayojengwa katika shule za Msingi Mwenge, Town School na Ipuli ili wajumbe wajiridhishe na gharama za ujenzi zilizotumika

10. Mkandarasi Luganyila Company Ltd anayetengeneza barabara Kata ya Cheyo Menejimenti imtake akaisawazishe barabara hiyo ili iweze kupitika wakati wote

11. "Site Meeting" kwa ajili ya kutambulisha miradi mbalimbali inayotekelezwa na Halmashauri iwe inafanyika na Wahe. Madiwani washirikishwe pamoja na Viongozi wengi (Wenyeviti wa Mitaa/Vijiji na Watendaji)

12. Menejimenti ijibu hoja zote ambazo hazijafungwa na Mkaguzi wa ndani katika kipindi cha siku kumi na nne (14)

13. Menejimenti ijenge choo katika jengo la Kitega Uchumi cha Halmashauri, Aidha choo hicho kigawanywe katika maeneo mawili
    (i) Sehemu moja iwe kwa ajili ya wafanya biashara waliopanga katika jengo hilo ambao hawatalipa chochote

    (ii) Sehemu ya pili iwe ni kwa ajili ya watu wengine ambao watalipia ili kupata huduma hiyo na Halmashauri kupata mapato.

14. Menejimenti iandae mafunzo ya wahe. madiwani na mapendekezo yake yawasilishwe kikao cha kamati ya fedha mwezi Machi 2017.

**TAMKO LA BARAZA LA MADIWANI KUHUSU MKOA KUSIMAMISHA WATUMISHI WA HALMASHAURI BILA MAMLAKA ZA NIDHAMU( KAMATI YA FEDHA NA BARAZA LA MADIWANI ) KUPEWA TAARIFA**

Baraza la madiwani lilijadili suala hili kwa kina na kutamka kwamba maamuzi ya Mkoa, baraza la madiwani halipingani nayo kinachotakiwa Mkoa ufuatie taratibu, kanuni na sheria kwa kuhakikisha mamlaka za nidhamu zinashirikishwa kwanza kabla ya hatua yoyote haijachukuliwa ya kumsimamisha mtumishi vinginevyo hali hiyo ikiendelea itasababishia Halmashauri yetu gharama zisizo za lazima hivyo baraza lilitaka Mkoa ufuate Kanuni na Sheria katika suala lolote linalohusu kushughulikia watumishi wanaotuhumiwa badala ya kuja na kutamka watumishi kadhaa wapumzishwe kazi.

TAARIFA FUPI TOKA KWA MKURUGENZI

Mkurugenzi manispaa alitumia nafasi hiyo kulijulisha baraza la madiwani kwamba mpaka sasa kuna watumishi wawili wamepumzishwa kazi kutokana na tuhuma mbalimbali.

watumishi hao ni :-

1) Bw. Deusdedit Ng'holombi - Afisa Manunuzi Halmashauri ya Manispaa , mtumishi huyu anatuhuma mbili:-

   (i)Ya kwanza toka Ofisi ya Katibu tawala Mkoa

   (ii) ya pili toka TAMISEMI

2) Bw. Paschal Barongo - Mratibu wa TASAF - Tayari barua imeshatoka Mkoani ambayo inamtuhumu kuhusiana na masuala ya malipo hewa kuhusiana na kaya masikini. Hata hivyo menejimenti imeshamrejesha kwenye kazi yake ya zamani Idara ya Uchumi.

Alisema taarifa kamili juu ya masuala haya itawasilishwa baada ya uchunguzi kukamilika.

MUHT: NA. MBM 4/2016/2017/13 KUFUNGA MKUTANO

Mwenyekiti alifunga Mkutano saa 9. 38 alasiri kwa kuwashukuru wajumbe wote kwa namna walivyochangia hoja kwa kila agenda na kufikia maamuzi. Alisisitiza maagizo yote yaliyotolewa na baraza yafanyiwe kazi hususani kuhakikisha kamati za maendeleo zinabaini haraka vyanzo vya mapato ikiwezekana ndani ya mwezi mmoja na nusu iwe tayari na taarifa iwasilishwe kamati ya fedha na baraza la madiwani.

Alihitimisha kwa kutoa taarifa ya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora kufutiwa tozo ya faini ya Tshs 12,000,000/= baada ya yeye kukata rufaa kwa Mhe. waziri wa nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumuomba atengue uamuzi uliotolewa na baraza la hifadhi na usimamizi wa mazingira wa kuitoza Halmashauri yetu faini ya Tshs 12,000,000/=

MUHTASARI UMETHIBITISHWA NA

| | |
|---|---|
| Bosco O. Ndunguru | L.C.Ulaya |
| KATIBU | MWENYEKITI |
| SAHIHI ............ | SAHIHI ................ |
| TAREHE ....24/05/2017.... | TAREHE:....24/05/2017.... |